

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA.
HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA.**

SHULE YA SEKONDARIUCHINDILE
S.L P 135
MLIMBA.

TAREHE.....

KUMB. NA.....
MWANAFUNZI.....
S.L.P.....

**YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI UCHINDILE
WILAYA YA MLIMBA MWAKA 2021.**

1.0 Nafurahi kukuarifu/kukujulisha wewe.....

Mwenye namba ya mtihani..... kutoka shule ya msingi.....
Kuwa umebahatika kuchaguliwa kwa mafunzo ya Elimu ya sekondari kidato cha kwanza
katika shule hii kwa mwaka..... baada ya kufaulu mtihani wa Elimu ya
msingi.Unatakiwa kuripoti shulen i tarehe..... mwisho wa kuripoti
ni tarehe.....

2.0 MAHITAJI YA MWANAFUNZI

1. Sare za shule hii kwa wavulana ni suruali 2 za kijani jeshi na mashati meupe 2 ya mikono mifupi tetro ni sketi 2 za kijani jeshi na mashati meupe 2 ya mikono mifupi tetro ni kwa wasichana.
2. Kwa wanafunzi wa kiislamu wa kike waje na mashati nusu kanzu meupe 2 ya mikono mirefu,hijabu 2 nyeupe na sketi ndefu 2 za kijani jeshi.
3. Viatu vyeusi vya kamba na soksi nyeupe.
4. Sare za michezo ni Track suit rangi ya bluu,pamoja na raba za michezo.
5. Daftari kubwa 10 counter book quire two,mkebe,rula na penseli.
6. Jembe jipya lenye mpini,fyekeo,ndoo lita kumi na fagio.
7. Tai rangi ya kitambaa cha sketi au suruali.
8. Faili (spring file)

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya elimu Na.25 ya mwaka 1978.Aidha inazingatia miongozo yote itolewayo na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo.

1.SHERIA ZA JUMLA:

- (a)Heshima kwa walimu wote,viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b)Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- (c)Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation) na kazi ulizopewa na walimu.
- (d)Kuwahi katika kila shughuli za shule na zingine utakazopewa.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (f)Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- (g)Kuvaa sare rasmi za shule wakati wote unapotakiwa.
- (h)Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

2.MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE BILA ONYO.

- (a) Wizi.
- (b) Uasherati.
- (c) Ubakaji.
- (d) Ulevi na matumizi ya madwa ya kulevyta kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi, kubeli n.k
- (e) Kupiga au kupigana.
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali ya uma.
- (g) Kudharau bendera ya taifa.
- (h) Kuoa au kuolewa
- (i) Kupata mimba.
- (j) Kutoa mimba,kuharibu mimba au kusaidia utoaji mimba.
- (k) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule na watu.
- (l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- (m)Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

Tafadhalii soma kwa makini maagizo/maelezo haya na uyatekeleze kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....
RONALD JOHN SIKAPONDA
MKUU WA SHULE.